

**Minutes of meeting of Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam
1st April 2006**

Attendance

Elaine Baker
Frank Mwasa
Ibrahim Kizyara
Mejah Mbuya
Salum Chimburumburu
Selemani Alonasi
Sosthenes Amlima
Kharidi Shabani

Jukwaa la Jamii Tanzania

UWABA ilishiriki kwenye jukwaa la Jamii Tanzania tarehe 22 hadi 25 machi Mnazi Mmoja. Iliripotiwa kuwa tulikuwa na kibanda kilichokuwa na bango kubwa lililotengenezwa na Sosthenes, na kuwa wanachama wengine akiwemo Juma, Shukuru, Ibrahim na Elaine walihudhuria. Iliripotiwa kwamba wengi waliohudhuria wakiwemo wageni maalum, walivutiwa na UWABA. Tulifanya mawasiliano na mashirika mengine yasiyokuwa ya serikali, akiwemo Leonard Magwayega wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, aliyesema angetoa mada juu ya sheria za barabarani kama zanalyotumika kwa wapanda baisikeli. Tuliwasiliana pia na PELO (Shirika la Ukuzaji Mahusiano ya Ki-elimu) ambalo lingependa kuandaa nafasi kwetu ya kuongea na wanafunzi kuhusu upandaji wa baisikeli. Picha ya kibanda chetu ilipitishwa kwa wajumbe wakati wa kikao.

Mkutano na AALCOM

Mejah na Elaine waliripoti kutembelea ofisi za AALCOM, shirika jingine lisilo la kiserikali linalojihusisha na usafirishaji. Shirika hili lina wanachama ishirini, wengi wao wakiwa ni wataalam katika nyanja/sekta ya usafirishaji. Mwenyekiti wao ni profesa Majani ambaye ni mtalaam katika mipango miji na katibu Mtendaji ni bwana Mlamba ambaye ni mtalaam mshauri. Mkewe, bibi Mlamba ni msimamizi wa Mradi wa Mabasi yaendayo Kasi wa Jiji la Dar es Salaam. Mtu ambaye Elaine na Mejah walikutana nae ni Prosper Nyaki mfanyakazi wa shirika.

AALCOM imekuwa ikikua tangu mwaka 2003. Miongoni mwa kazi zilizofanywa na AALCOM ni kukagua idadi ya watu wanaotumia aina mbalimbali za usafiri Dar es Salaam, inayoonesha 45% wanasafiri kwa miguu au baisikeli, 43% kwa basi, 6% usafiri binafsi na 6% ni njia zinginezo za usafiri. Pia husambaza baisikeli za California. Pia waliandaa mpango wa kukuza matumizi ya baisikeli jijini Dar es salaam.

Kazi walizopanga kwa badae ni kuwa na msafara wa baiskeli au vikundi vya wapanda baiskeli, kukodisha baiskeli kwa wafanyakazi wa shirika, kuandaa mikakati na kushughulikia maswala ya usalama barabarani na maegesho.

Mejah alifafanua kuwa UWABA ishirikiane na AALCOM katika mambo yanayowaunganisha. Mashirika yatatoa msaada zaidi kwa kuwa AALCOM ni kundi la wataalam ambao wengi wao hawapandi baiskeli kama njia ya usafiri wakati UWABA ina wapanda baiskeli ambao ni wanachama.

Mengineyo

Mejah aliripoti kuwa aligongwa akiwa amepanda baiskeli na kuongea na askari wa usalama barabarani ambaye aliunga mkono kazi za UWABA.

Mejah alipendekeza ufanyike mdahalo wa televisheni kuhusu mambo ya usafiri na UWABA itashiriki . Pia alisema anawafahamu watu wanaofanya kazi kwenye televisheni ambao watasaidia kufanikisha kazi hii.

Wanachama walitaka viandaliwe vitambulisho na nembo

Ilikubalika kuwa moja ya vipaumbela vya badae vya UWABA iwe ni kufanya vikao na mamlaka husika ya serikali.